

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA



VACANCIES

Article 129 (1) (a) of the Constitution of the United Republic of Tanzania, 1977 in Chapter six, Part I, establishes the Commission for Human Rights and Good Governance (CHRAGG). Following the expiry of the tenure of Commissioners, the Appointment Committee for Appointments of Commissioners, established under Article 129 (4) of the Constitution of the United Republic of Tanzania, 1977, do hereby invites applications from suitably qualified Tanzania citizens to apply for the posts of Chairperson, Vice Chairperson, Commissioners and Assistant Commissioners in the Commission for Human Rights and Good Governance as follows:-

1. POST: CHAIRMAN (1POST)

1.1 Qualifications

According to Article 129 (2) of the Constitution of the United Republic of Tanzania, 1977 an applicant shall be a person who possess qualifications for appointment as a Judge.

1.2 Required Experience

In accordance to regulation 4 (4) (a – i) of the CHRAGG (Appointments Procedure for Commissioners) Regulations, 2018 the applicant shall have: -

- a. Knowledge, experience and considerable degree of involvement in matters relating to law, governance, politics or social affairs;
- b. The highest reputation known for his/her morality, integrity, impartiality and competence in matters of human rights and good governance;

- c. Strong commitment to human rights norms and values;
- d. Excellent writing and communication skills in both English and Swahili;
- e. Ability to balance rights and to make fair and sound decision expeditiously, and to articulate them in writing or orally;
- f. Capacity to handle emotionally difficult and challenging situations with tact and diplomacy;
- g. Capacity to handle delicate social and political situations and complaints with confidentiality, where necessary;
- h. Strong conflict resolution skills; and
- i. Ability to work effectively as a team member, as well as alone.

1.3 Duties

- a. To sensitize countrywide about preservation of human rights and duties to the public in accordance with the Constitution and the laws of the land;
- b. To receive complaints in relation to violation of human rights in general;
- c. To conduct inquiry on matters relating to infringement of human rights and violation of principles of good governance;
- d. To conduct research, to impart or disseminate to the public countrywide education in respect of human rights and good governance;
- e. If necessary, to institute proceedings in court in order to prevent violation of human rights or to restore a right that was caused by that infringement of human rights, or violation of principles of good governance;

- f. Inquire into the conduct of any person concerned and any institution concerned in relation to the ordinary performance of his duties or functions or abuse of the authority of his office;
- g. To advice the Government and other public Institutions and private sector in respect of human rights and good governance; and
- h. To take necessary action in order to promote and enhance conciliation and reconciliation among persons and various institutions appearing or being brought before the CHRAGG.

1.4 Salary Grade

Salary at a scale of LSSE/8 -1 and additional attractive fringe benefits.

2. POST: VICE CHAIRMAN (1 POST)

2.1 Qualifications

According to Article 129 (2) (c) of the Constitution of United Republic of Tanzania, 1977 applicant should possess skills, experience and wide knowledge in matters relating to human rights, law, administration, political or social affairs.

2.2 Required Experience

In accordance to regulation 4 (4) (a – i) of the CHRAGG (Appointments Procedure for Commissioners) Regulations, 2018 the applicant shall have: -

- a. Knowledge, experience and considerable degree of involvement in matters relating to law, governance, politics or social affairs;
- b. The highest reputation known for his/her morality, integrity, impartiality and competence in matters of human rights and good governance;
- c. Strong commitment to human rights norms and values;
- d. Excellent writing and communication skills in both English and Swahili;

- e. Ability to balance rights and to make fair and sound decision expeditiously, and to articulate them in writing or orally;
- f. Capacity to handle emotionally difficult and challenging situations with tact and diplomacy;
- g. Capacity to handle delicate social and political situations and complaints with confidentiality, where necessary;
- h. Strong conflict resolution skills; and
- i. Ability to work effectively as a team member, as well as alone.

2.3 Duties

- a. To sensitize countrywide about preservation of human rights and duties to the public in accordance with the Constitution and the laws of the land;
- b. To receive complaints in relation to violation of human rights in general;
- c. To conduct inquiry on matters relating to infringement of human rights and violation of principles of good governance;
- d. To conduct research, to impart or disseminate to the public countrywide education in respect of human rights and good governance;
- e. If necessary, to institute proceedings in court in order to prevent violation of human rights or to restore a right that was caused by that infringement of human rights, or violation of principles of good governance;
- f. Inquire into the conduct of any person concerned and any institution concerned in relation to the ordinary performance of his duties or functions or abuse of the authority of his office;
- g. To advice the Government and other public Institutions and private sector in respect of human rights and good governance; and

- h. To take necessary action in order to promote and enhance conciliation and reconciliation among persons and various institutions appearing or being brought before the Commission.

2.4 Salary Grade

Salary at a scale of LSSE/7-1 and additional attractive fringe benefits.

3. POST: COMMISSIONERS (5 POSTS)

3.1 Qualifications

According to Article 129 (2) (c) of the Constitution of United Republic of Tanzania, 1977 applicant should possess skills, experience and wide knowledge in matters relating to human rights, law, administration, political or social affairs.

3.2 Required Experience

In accordance to regulation 4 (4) (a – i) of the CHRAGG (Appointments Procedure for Commissioners) Regulations, 2018 the applicant shall have: -

- a. Knowledge, experience and considerable degree of involvement in matters relating to law, governance, politics or social affairs;
- b. The highest reputation known for his/her morality, integrity, impartiality and competence in matters of human rights and good governance;
- c. Strong commitment to human rights norms and values;
- d. Excellent writing and communication skills in both English and Swahili;
- e. Ability to balance rights and to make fair and sound decision expeditiously, and to articulate them in writing or orally;

- f. Capacity to handle emotionally difficult and challenging situations with tact and diplomacy;
- g. Capacity to handle delicate social and political situations and complaints with confidentiality, where necessary;
- h. Strong conflict resolution skills; and
- i. Ability to work effectively as a team member, as well as alone.

3.3 Duties

- a. To sensitize countrywide about preservation of human rights and duties to the public in accordance with the Constitution and the laws of the land;
- b. To receive complaints in relation to violation of human rights in general;
- c. To conduct inquiry on matters relating to infringement of human rights and violation of principles of good governance;
- d. To conduct research, to impart or disseminate to the public countrywide education in respect of human rights and good governance;
- e. If necessary, to institute proceedings in court in order to prevent violation of human rights or to restore a right that was caused by that infringement of human rights, or violation of principles of good governance;
- f. Inquire into the conduct of any person concerned and any institution concerned in relation to the ordinary performance of his duties or functions or abuse of the authority of his office;
- g. To advice the Government and other public Institutions and private sector in respect of human rights and good governance; and

- h. To take necessary action in order to promote and enhance conciliation and reconciliation among persons and various institutions appearing or being brought before the Commission.

3.4 Salary Grade

Salary at a scale of LSSE/6-1 and additional attractive fringe benefits.

4. POST: ASSISTANT COMMISSIONERS

4.1 Qualifications

According to section 7 (3) of the CHRAGG Act, Cap. 391 the Applicant should have highest reputation and known for his high morality, integrity, impartiality and competence in matters of human rights and good governance.

4.2 Required Experience

In accordance to regulation 4 (4) (a – i) of the CHRAGG (Appointments Procedure for Commissioners) Regulations, 2018 the applicant shall have: -

- a. Knowledge, experience and considerable degree of involvement in matters relating to law, governance, politics or social affairs;
- b. The highest reputation known for his/her morality, integrity, impartiality and competence in matters of human rights and good governance;
- c. Strong commitment to human rights norms and values;
- d. Excellent writing and communication skills in both English and Swahili;
- e. Ability to balance rights and to make fair and sound decision expeditiously, and to articulate them in writing or orally;
- f. Capacity to handle emotionally difficult and challenging situations with tact and diplomacy;

- g. Capacity to handle delicate social and political situations and complaints with confidentiality, where necessary;
- h. Strong conflict resolution skills; and
- i. Ability to work effectively as a team member, as well as alone.

4.3 Duties

- a. Receive complaints from the public;
- b. Make such on-the-spot investigation as may be necessary; and
- c. Discharge any other duties relating to the functions of the CHRAGG as may be assigned to him by the CHRAGG.

4.4 Salary Grade

Salary at a scale of **LSSE4** and additional attractive fringe benefits.

5. OTHER MATTERS FOR CONSIDERATION

5.1 TENURE AND CONDITIONS OF SERVICE

According to Article 129 (5) of the Constitution of the United Republic of Tanzania, 1977, Chairman, Vice Chairman and all other Commissioners, shall each hold office for a period of three years (3) and may be re-appointed for another only one term of three years (3).

Also, Article 129 (6), of the Constitution of United Republic of Tanzania, 1977 read together with Section 9 (1) of the CHRAGG Act, Cap. 391, for purposes of protection of Commissioners from conflict of interests, any person who is appointed as Commissioner of CHRAGG shall immediately abandon any office held by him in any political party or other office: member of Parliament; the office of member of the Zanzibar House of Representatives; the office of Speaker of the National Assembly; the office of Speaker of the Zanzibar House of Representative; the office of Judge or other judicial office; any office in the Public Service; the office of member of an Electoral Commission; the office of member of a local government authority and any office in the service of any local government authority;

any other public office.

5.2 MODE OF APPLICATIONS

Application letters accompanied with comprehensive Curriculum Vitae, copies of educational qualifications, three letters of recommendation, shall be forwarded by post to the Appointment Committee, Utumishi Street, Government City, Mtumba Area P.O Box. 1954 Dodoma; or by email kamati.uteuzi@oag.go.tz. For applicants in Tanzania Mainland who wish to submit in person, letters should be submitted to the Office of the Attorney General's Building, Utumishi Street, Government City, Mtumba Area, Dodoma. For applicants from Zanzibar who wish to submit in person, letters should be submitted in person to the Offices of the Commission for Human Rights and Good Governance, located at Shehia ya Mombasa, Mkapa Road, Tawin Street, Building No. MS/ML/F199, Magharibi B. District within Mjini Magharibi Region.

The deadline for submission of applications shall be 21 days from the date of first publication of this advertisement on or before 31 August, 2026.

5.3 NOTIFICATION AND PUBLICATION OF SHORTLISTED APPLICANTS:

According to rule 6 (5) of the CHRAGG (Appointments Procedure for Commissioners) Regulations, 2018, the names of short-listed applicants shall be published in the media and members of the public shall be invited to submit to the Appointment Committee, Utumishi Street, Government City, Mtumba Area P.O Box. 1954 Dodoma; email: kamati.uteuzi@oag.go.tz, within a period of twenty one (21) days, comments they consider relevant to the suitability of any of the short-listed applicants. The Appointments Committee may consider comments received from members of the public.

Short-listed applicants will be notified on the date and place where interview will be conducted by the Appointments Committee.

For any inquiries please contact through Telephone Number 0733122200.

Issued by:

**DEPUTY ATTORNEY GENERAL
THE SECRETARY
APPOINTMENTS COMMITTEE**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TANGAZO LA NAFASI ZA UTEUZI

Ibara ya 129 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 katika Sura ya Sita, Sehemu ya Kwanza inaanzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB). Kwa kuwa muda wa kuhudumu wa Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora umefika mwisho, Kamati ya Uteuzi iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 129 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba kujaza nafasi wazi ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Makamishna na Makamishna Wasaidizi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kama ifuatavyo:-

1. NAFASI: MWENYEKITI (NAFASI 1)

1.1 Sifa za Mwombaji:-

Kwa mujibu wa Ibara ya 129 (2) (a), ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 mwombaji atakuwa ni mtu mwenye sifa ya kuweza kuteuliwa kuwa Jaji;

1.2 Uzoefu Unaohitajika

Kwa kuzingatia kanuni ya 4 (4) (a – i), ya Kanuni za THBUB (Utaratibu wa Uteuzi wa Makamishna), 2018 mwombaji anatakiwa kuwa na:-

- a. Maarifa, uzoefu na ushiriki katika masuala yanayohusiana na sheria, utawala, siasa na mambo ya kijamii;
- b. Sifa za hali ya juu zinazohusiana na maadili, uadilifu, kutokuwa na upendeleo na kuwa mahiri kwenye masuala ya haki za binadamu na utawala bora;

- c. Kujitoa kwa hali ya juu kwenye masuala ya haki za binadamu na maadili;
- d. Uwezo na ujuzi mkubwa wa kuandika na kuongea Kiswahili na Kiingereza fasaha;
- e. Uwezo wa kuwa na mizania inayolingana katika masuala ya haki na kutenda bila upendeleo na kutoa maamuzi sahihi kwa haraka na awe na uwezo wa kuyaandika na kuyasema;
- f. Uwezo wa kushughulikia hali ngumu na zenye changamoto za kihisia kwa busara na ustadi wa kidiplomasia;
- g. Uwezo wa kushughulikia masuala nyeti ya kijamii, kisiasa na malalamiko kwa usiri inapohitajika;
- h. Ujuzi wa hali ya juu wa kutatua migogoro; na
- i. Uwezo wa kufanya kazi ipasavyo kwa ushirikiano na binafsi.

1.3 Majukumu

- a. Kuhamasisha nchini hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi;
- b. Kufanya shughuli za kupokea malalamiko ya uvunjaji wa haki za binadamu kwa jumla;
- c. Kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;
- d. Kufanya utafiti, kutoa na kueneza nchini elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na utawala bora;
- e. Kama ikibidi, kufungua mashauri mahakamani ili kuzuia vitendo vya uvunjaji wa haki za binadamu au kurekebisha haki inayotokana na uvunjwaji huo wa haki za binadamu, au ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;

- f. Kuchunguza mwenendo wa mtu yeyote anayehusika au taasisi yoyote inayohusika katika utekelezaji wa kawaida wa madaraka ya kazi au majukumu yake au utekelezaji unaokiuka madaraka hayo;
- g. Kutoa ushauri kwa Serikali na vyombo vingine vya umma na vya sekta ya binafsi kuhusu haki za binadamu na utawala bora;
- h. Kuchukua hatua zipasazo kwa ajili ya kukuza na kuendeleza usuluhishi na suluhu miongoni mwa watu na taasisi mbalimbali wanaofika au kufikishwa mbele ya Tume.

1.4 Ngazi ya Mshahara:

Kiwango cha LSSE/8 -1 na kupatiwa nyongeza ya kuvutia na motisha.

2. NAFASI: MAKAMU MWENYEKITI (NAFASI 1)

2.1 Sifa za Mwombaji

Kwa mujibu wa Ibara ya 129 (2) (c), ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 mwombaji anatakiwa awe mtu mwenye ujuzi, uzoefu na upeo mkubwa katika mambo ya haki za binadamu, sheria, utawala, siasa au mambo ya jamii.

2.2 Uzoefu Unaohitajika

Kwa kuzingatia kanuni ya 4 (4) (a – i), ya Kanuni za THBUB (Utaratibu wa Uteuzi wa Makamishna), 2018 mwombaji anatakiwa kuwa na:-

- a. Maarifa, uzoefu na ushiriki katika masuala yanayohusiana na sheria, utawala na mambo ya kijamii;
- b. Sifa za hali ya juu zinazohusiana na maadili, uadilifu, kutokuwa na upendeleo na kuwa mahiri kwenye masuala ya haki za binadamu na utawala bora;
- c. Kujitoa kwa hali ya juu kwenye masuala ya haki za binadamu na maadili;

- d. Uwezo na ujuzi mkubwa wa kuandika na kuongea Kiswahili na Kiingereza fasaha;
- e. Uwezo wa kuwa na mizania inayolingana katika masuala ya haki na kutenda bila upendeleo na kutoa maamuzi sahihi kwa haraka na awe na uwezo wa kuyaandika na kuyasema;
- f. Uwezo wa kushughulikia hali ngumu na zenye changamoto za kihisia kwa busara na ustadi wa kidiplomasia;
- g. Uwezo wa kushughulikia masuala nyeti ya kijamii, kisiasa na malalamiko kwa usiri inapohitajika;
- h. Ujuzi wa hali ya juu wa kutatua migogoro; na
- i. Uwezo wa kufanya kazi ipasavyo kwa ushirikiano na binafsi.

2.3 Majukumu:

- a. Kuhamasisha nchini hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi;
- b. Kufanya shughuli za kupokea malalamiko ya uvunjaji wa haki za binadamu kwa jumla;
- c. Kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;
- d. Kufanya utafiti, kutoa na kueneza nchini elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na utawala bora;
- e. Kama ikibidi, kufungua mashauri mahakamani ili kuzuia vitendo vya uvunjaji wa haki za binadamu au kurekebisha haki inayotokana na uvunjwaji huo wa haki za binadamu, au ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;

- f. Kuchunguza mwenendo wa mtu yeyote anayehusika au taasisi yoyote inayohusika katika utekelezaji wa kawaida wa madaraka ya kazi au majukumu yake au utekelezaji unaokiuka madaraka hayo;
- g. Kutoa ushauri kwa Serikali na vyombo vingine vya umma na vya sekta ya binafsi kuhusu haki za binadamu na utawala bora; na
- h. Kuchukua hatua zipasazo kwa ajili ya kukuza na kuendeleza usuluhishi na suluhu miongoni mwa watu na taasisi mbalimbali wanaofika au kufikishwa mbele ya Tume.

2.4 Ngazi ya Mshahara

Kiwango cha LSSE/7 -1 na kupatiwa nyongeza ya kuvutia na motisha.

3. NAFASI: MAKAMISHNA (NAFASI 5)

3.1 Sifa za Mwombaji:-

Kwa mujibu wa Ibara ya 129 (2) (c), ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 mwombaji anatakiwa awe mtu mwenye ujuzi, uzoefu na upeo mkubwa katika mambo ya haki za binadamu, sheria, utawala, siasa au mambo ya jamii.

3.2 Uzoefu Unaohitajika

Kwa kuzingatia kanuni ya 4 (4) (a – i), ya Kanuni za THBUB (Utaratibu wa Uteuzi wa Makamishna), 2018 mwombaji anatakiwa kuwa na:-

- a. Maarifa, uzoefu na ushiriki katika masuala yanayohusiana na sheria, utawala na mambo ya kijamii;
- b. Sifa za hali ya juu zinazohusiana na maadili, uadilifu, kutokuwa na upendeleo na kuwa mahiri kwenye masuala ya haki za binadamu na utawala bora;
- c. Kujitoa kwa hali ya juu kwenye masuala ya haki za binadamu na maadili;

- d. Uwezo na ujuzi mkubwa wa kuandika na kuongea Kiswahili na Kiingereza fasaha;
- e. Uwezo wa kuwa na mizania inayolingana katika masuala ya haki na kutenda bila upendeleo na kutoa maamuzi sahihi kwa haraka na awe na uwezo wa kuyaandika na kuyasema;
- f. Uwezo wa kushughulikia hali ngumu na zenye changamoto za kihisia kwa busara na ustadi wa kidiplomasia;
- g. Uwezo wa kushughulikia masuala nyeti ya kijamii, kisiasa na malalamiko kwa usiri inapohitajika;
- h. Ujuzi wa hali ya juu wa kutatua migogoro; na
- i. Uwezo wa kufanya kazi ipasavyo kwa ushirikiano na binafsi.

3.3 Majukumu:-

- a. Kuhamasisha nchini hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi;
- b. Kufanya shughuli za kupokea malalamiko ya uvunjaji wa haki za binadamu kwa jumla;
- c. Kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;
- d. Kufanya utafiti, kutoa na kueneza nchini elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na utawala bora;
- e. Kama ikibidi, kufungua mashauri mahakamani ili kuzuia vitendo vya uvunjaji wa haki za binadamu au kurekebisha haki inayotokana na uvunjwaji huo wa haki za binadamu, au ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;

- f. Kuchunguza mwenendo wa mtu yeyote anayehusika au taasisi yoyote katika utekelezaji wa kawaida wa madaraka ya kazi au majukumu yake au utekelezaji unaokiuka madaraka hayo;
- g. Kutoa ushauri kwa Serikali na vyombo vingine vya umma na vya sekta ya binafsi kuhusu haki za binadamu na utawala bora;
- h. Kuchukua hatua zipasazo kwa ajili ya kukuza na kuendeleza usuluhishi na suluhu miongoni mwa watu na taasisi mbalimbali wanaofika au kufikishwa mbele ya Tume.

3.4 Ngazi ya Mshahara:-

Kiwango cha LSSE/6 -1 na kupatiwa nyongeza ya kuvutia na motisha.

4. NAFASI: MAKAMISHNA WASAIDIZI

4.1 Sifa za Mwombaji

Kwa mujibu wa kifungu cha 7 (3) cha Sheria ya THBUB Sura ya 391 mwombaji anatakiwa awe mtu mwenye sifa njema na anafahamika kwa kuwa mwenye maadili ya juu, uadilifu, kutopendela na mahiri katika masuala ya haki za binadamu na utawala bora.

4.2 Uzoefu Unaohitajika

Kwa kuzingatia kanuni ya 4 (4) (a – i), ya Kanuni za THBUB (Utaratibu wa Uteuzi wa Makamishna), 2018 mwombaji anatakiwa kuwa na:-

- a. Maarifa, uzoefu na ushiriki katika masuala yanayohusiana na sheria, utawala na mambo ya kijamii;
- b. Sifa za hali ya juu zinazohusiana na maadili, uadilifu, kutokuwa na upendeleo na kuwa mahiri kwenye masuala ya haki za binadamu na utawala bora;
- c. Kujitoa kwa hali ya juu kwenye masuala ya haki za binadamu na maadili;

- d. Uwezo na ujuzi mkubwa wa kuandika na kuongea Kiswahili na Kiingereza fasaha;
- e. Uwezo wa kuwa na mizania inayolingana katika masuala ya haki na kutenda bila upendeleo na kutoa maamuzi sahihi kwa haraka na awe na uwezo wa kuyaandika na kuyasema;
- f. Uwezo wa kushughulikia hali ngumu na zenye changamoto za kihisia kwa busara na ustadi wa kidiplomasia;
- g. Uwezo wa kushughulikia masuala nyeti ya kijamii, kisiasa na malalamiko kwa usiri inapohitajika;
- h. Ujuzi wa hali ya juu wa kutatua migogoro; na
- i. Uwezo wa kufanya kazi ipasavyo kwa ushirikiano na binafsi.

4.3 Majukumu

- a. Kupokea malalamiko kutoka kwa umma;
- b. Kufanya uchunguzi wa papo hapo kama inavyoweza kuhitajika; na
- c. Kutekeleza kazi nyingine zinazohusiana na majukumu ya THBUB kama atakavyopangiwa na THBUB.

4.4 Ngazi ya Mshahara

Kiwango cha LSSE4 na kupatiwa nyongeza ya kuvutia na motisha.

5. MASUALA MENGINE YA KUZINGATIA

5.1 MUDA NA MASHARTI YA KAZI

- a. Kwa kuzingatia Ibara ya 129 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wengine wote, kila mmoja atashika madaraka yake

kwa kipindi cha miaka mitatu (3) na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja tu cha miaka mitatu (3);

- b. Vilevile, Ibara ya 129 (6) ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, 1977 ikisomwa pamoja na Kifungu cha 9 (1) cha Sheria ya THBUB, Sura ya 391, inaelekeza kuwa, kwa madhumuni ya kuwakinga Makamishna kutokana na migongano ya kimaslahi, mtu yeyote akiteuliwa kuwa Kamishna wa THBUB atalazimika kuacha mara moja madaraka yoyote katika chama chochote cha siasa, au madaraka ya aina nyingine yoyote kama vile: Ubunge; Ujumbe katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar; Spika wa Bunge; Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar; Jaji au wadhifa mwingine wa kimahakama; Utumishi Serikalini; Ujumbe wa Tume ya Uchaguzi; Ujumbe katika mamlaka ya Serikali za Mitaa na utumishi wowote katika mamlaka ya serikali za mtaa; au nafasi yoyote nyingine katika utumishi wa umma.

5.2 NAMNA YA KUOMBA

Barua zote za maombi zinapaswa kuambatana na wasifu wa kina, nakala za vyeti vya taaluma/elimu na barua tatu za mapendekezo kutoka kwa wadhamini ambazo zitatumwa kwa Kamati ya Uteuzi, Mtaa wa Utumishi, Mji wa Serikali Eneo la Mtumba, S. L. P. 1954, Dodoma, au barua pepe: kamati.uteuzi@oag.go.tz. Kwa watakaowasilisha kwa mkono, kwa upande wa Tanzania Bara barua zitapokelewa Jengo la Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali zilizopo Mtaa wa Utumishi, Mji wa Serikali Eneo la Mtumba Dodoma. Aidha, kwa upande wa Zanzibar barua zitawasilishwa kwa mkono katika Ofisi za Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora zilizopo Shehia ya Mombasa Barabara ya Mkapa Mtaa wa Tawin Jengo Na.MS/ML/F199 Wilaya ya Magharibi B, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha maombi itakuwa siku 21 tangu tarehe ya kwanza ya kutangazwa kwa Tangazo hili, yaani, kabla au ifikapo tarehe 31 Agosti, 2026.

5.3 TAARIFA NA UCHAPISHAJI WA MAJINA YA WAOMBAJI WALIOKIDHI VIGezo

Kwa mujibu wa Kanuni ya 7(1) ya Kanuni za THBUB (Utaratibu wa Uteuzi wa Makamishna), 2018 majina ya waombaji wote waliokidhi vigezo na kuitwa kwenye usaili yatatangazwa kwenye vyombo vya habari ambapo umma utaalikwa kuwasilisha maoni kwa Kamati ya Uteuzi, Mtaa wa Utumishi, Mji wa Serikali Eneo la Mtumba, S. L. P. 1954, Dodoma, au barua pepe: kamati.uteuzi@oag.go.tz ndani ya siku ishirini na moja, (21) iwapo waombaji wanastahili kushika nafasi hizo. Kamati ya Uteuzi inaweza kuzingatia maoni yaliyowasilishwa kutoka kwa umma.

Waombaji waliokidhi vigezo watajulishwa tarehe na mahala watakapofanyiwa usaili na Kamati ya Uteuzi.

Kwa ufafanuzi wowote piga simu namba 0733122200.

Imetolewa na:

**NAIBU MWANASHERIA MKUU
KATIBU
KAMATI YA UTEUZI**